TANGAZO LA SERIKALI NA. 80 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1)(2) na 14)*

NOTISI YA MPANGO WA UENDELEZAJI UPYA ENEO LA SINZA YA MWAKA 2025

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Mpango wa Uendelezaji Upya Eneo la Sinza ya Mwaka 2025.

Mpango wa uendelezaji upya wa Ardhi ya eneo la Sinza
Sura ya 355

2. Eneo la Sinza kama lilivyoainishwa katika Jedwali linatangazwa kuwa eneo la Mpango wa Uendelezaji Upya kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji.

Mpango wa uendelezaji

3. Mipango ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Mpango wa uendelezaji upya eneo la Sinza ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye makutano ya barabara ya Sam Nujoma na Daraja la Mto Ng'ombe yenye majira – nukta 523002.7E, 9249725.84N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kuelekea barabara ya Sam Nujoma kwa umbali wa kilomita 2.7 hadi kwenye makutano ya barabara ya Sinza Mori ambao ni mpaka kati ya Manispaa ya Kinondoni na Manispaa ya Ubungo kwenye majira – nukta 524625.09E, 9251872.27N; baada ya hapo mpaka unaelekea barabara ya Sinza Mori kwa umbali wa kilomita 1.78 hadi kwenye majira – nukta 525626.3E, 9250555.85N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.58 hadi unapokutana na mkondo wa maji usiokuwa na jina hadi kwenye majira – nukta 5258243.638E, 9250169.004N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa kwenye mkondo wa maji usiokuwa na jina hadi unapokutana na Mto Ng'ombe kwenye majira – nukta 525794.469E, 9250031.276N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kufuata mto Ng'ombe umbali wa kilomita 8 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
28 Januari, 2025

DEOGRATIUS J. NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*